TOLEO LA DISEMBA 2025

MWENGE GOSPEL RUNNERS

# WAKIMBIZA INJILI



*Mch. Antipas akiubiri katika moja ya mikutano ya injili*

## YALIYOMO

Karibu katika toleo letu la Desemba 2025 la Jarida la Wakimbiza Injili T.A.G  Mwenge.

Katika toleo hili, tunaangazia mafanikio makubwa ya timu yetu ya 'Mwenge Gospel Runners' iliyofanikiwa kuwavuna watu 326 kwa Kristo katika mikoa ya Tabora, Singida, na Tanga.

Ungana nasi kushuhudia uponyaji wa ajabu, ukombozi wa kimbingu, na maono mapya ya mikakati ya injili inayotupeleka mwaka 2026 kwa ushindi mkuu

## HABARI ZA INJILI

### Mwenge Gospel Runners' Yatikisa Tabora, Singida na Tanga 2025

***Na Elizabeth Reuben, Mwenge***

TIMU ya uinjilisti ya Kanisa letu la TAG Mwenge Christian Centre (MCC), ijulikanayo kama Mwenge Gospel Runners, imehitimisha programu yake ya mwaka 2025 kwa mafanikio makubwa baada ya kuwaleta watu 326 kwa Kristo kupitia mikutano ya injili iliyofanyika katika mikoa mitatu nchini.

Mavuno hayo yamepatikana kupitia mikutano minane ya hadhara iliyoandaliwa mwezi Julai na Septemba katika mikoa ya Tabora, Singida, na Tanga.



*Mch. Antipas akiubiri katika moja ya mikutano ya injili*

Akizungumza na jarida hili, Mkuu wa Msafara wa timu hiyo, Ndugu Robson Lemgoha, alibainisha kuwa safari hiyo ya kimbingu haikuishia kwenye idadi ya watu waliookolewa tu, bali pia ilishuhudia uponyaji na ukombozi.

*Inaendelea ukurasawa Pili...*

*Inatoka ukurasa wa kwanza*

Katika mwaka huu 2025, tulifanikiwa kuhubiri mikutano minane na jumla ya watu waliookolewa pekee ni 326. Zaidi ya hapo, wengi walifunguliwa kutoka kwenye vifungo mbalimbali vya shetani," alisema Lemgoha.

## Maeneo yaliyofikiwa na takwimu za mavuno

Safari hiyo ya injili iligawanyika katika awamu mbili kuu. Awamu ya kwanza ilifanyika mwezi Julai 2025 mkoani Tabora (vijiji vya Mwakashanhara na Puge) na mkoani Singida (vijiji vya Ibaga na Ilongelo).

Awamu ya pili ilihitimishwa mwezi Septemba 2025 mkoani Tanga, ambapo timu ilifika katika vijiji vya Gharambo (Lushoto), Mkuzi (Muheza), Kwamba na Tunguli (Kilindi).

Mchanganuo wa nafsi zilizookolewa kwenye kila kituo ni kama ifuatavyo: Mwakashanhara 38, Puge 21, Ibaga 26, Ilongelo 16, Gharambo 114, Mkuzi 33, Kwamba 38 na Tunguli 40.

## Wito wa Mchungaji Kiongozi

Kwa upande wake, Mchungaji Kiongozi wa TAG Mwenge Christian Centre, Mch. Abdiel Mhini, ameeleza kufurahishwa kwake na kazi iliyofanywa na timu hiyo, huku akisisitiza kuwa kanisa hilo lina jukumu la kuwa kitovu cha uenezi wa injili.

Aidha, alitoa wito kwa kila mshirika wa TAG Mwenge kutambua kuwa anawajibika kibinafsi na Agizo Kuu la Bwana Yesu (Marko 16:15-18).

"Kila mshirika atambue kwamba yeye ni mmishenari na mwinjilisti. Bwana Yesu amegharimia wokovu wetu kwa damu ya msalaba, hivyo ni wajibu wa kila mmoja kuona moyoni mwake kuwa anapaswa kueneza injili ya Kristo," alisema Mch. Mhini.



**Mch. Abdiel Meshack Mhini**
Mchungaji Kiongozi
T.A.G Mwenge Christian Centre

# TAG MWENGE NA FALSAFA YA "KUSIHA MBEGU": WAVUNA NAFSI 236 MIKOANI MWAKA 2025

***Na Elizabeth Reuben, Mwenge.***

KANISA letu la TAG Mwenge Christian Centre (MCC) limefanikiwa kuwavuna watu 326 kwa Kristo ndani ya mwaka 2025 pekee, kupitia mikutano minane mikubwa ya injili iliyofanyika mikoani. Mafanikio haya yanatokana na falsafa mpya ya kanisa hili ya kujiona kama "kitalu cha kusia mbegu" za injili kwa ajili ya taifa.

*Inaendelea ukurasa wa pili...*

*Inatoka ukurasa wa pili*

Hatua hii ni utekelezaji wa vitendo wa Agizo Kuu la Bwana Yesu (Marko 16:15-18), na pia inaenda sambamba na mpango mkakati wa kitaifa wa miaka 13 wa Kanisa la TAG Tanzania, ujulikanao kama 'Moto wa Uamsho', ambao umejikita katika uinjilisti na umisheni.
Utekelezaji wa operesheni hizi unafanywa kupitia timu maalum ya injili ya kanisa hili, ijulikanayo kama 'Mwenge Gospel Runners'. Kati ya mwezi Julai na Septemba mwaka huu, timu hiyo iliweka kambi na kufanya mikutano katika mikoa ya Tabora, Singida na Tanga, na kufanikisha idadi hiyo ya waongofu wapya.

Akizungumza na gazeti hili kuhusu msukumo wa kazi hiyo, Mchungaji Kiongozi wa TAG MCC, Abdiel Meshack Mhini, alitumia taswira ya kilimo kuelezea wito wao mpya. "Sisi kama kanisa la mahali pamoja, ni kitalu cha kupanda mbegu ili zikiota zikapandwe maeneo mbalimbali zilete mavuno," alisema Mchungaji Mhini.

Aliendelea kumshukuru Mungu kwa matunda yaliyopatikana mwaka huu, akibainisha kuwa timu yao imefanya kazi kubwa ambapo watu wameokolewa, walioonewa na ibilisi wamewekwa huru, na waliofungwa na vifungo mbalimbali wamefunguliwa.

## Changamoto za Uwanjani

Pamoja na mafanikio hayo makubwa, safari hiyo haijakuwa tambarare. Timu ya injili imekuwa ikikumbana na changamoto mbalimbali za kiutendaji na kimazingira huko vijijini.

Mkuu wa msafara wa Mwenge Gospel Runners, Ndugu Robson Lemgoha, alibainisha changamoto ya maandalizi hafifu katika vituo vinavyohubiriwa injili. Alitaja ukosefu wa majukwaa kama kikwazo kikubwa, hali inayolazimu timu kuingia gharama za ziada za kuyatengeneza au wakati mwingine kulazimika kuhubiri bila jukwaa. Vilevile, vyombo vya muziki vimekuwa vikihitaji matengenezo ya mara kwa mara kutokana na mazingira magumu.
Lemgoha pia aligusia mgongano wa kimtazamo na baadhi ya wachungaji wenyeji, ambao hutaka mikutano ifanyike kwenye maeneo ya mikusanyiko ya watu wengi badala ya viwanja vya makanisa husika.



Ndg. Robson Lemgoha
Mkuu wa msafara

"Kama timu tumekuwa tukiwashauri wachungaji [wenyeji] kwa kuwapa faida za kufanyia mikutano hiyo kanisani, ikiwa ni pamoja na kulifanya kanisa lijulikane zaidi. Pia usalama kwa vyombo vya muziki unakuwa mkubwa kwa sababu tunalala kanisani," alifafanua Lemgoha.

## Kikwazo cha Kifedha

Mbali na changamoto za uwanjani, Mchungaji Mhini alibainisha kuwa upatikanaji wa fedha za kuendesha mikutano hiyo imekuwa changamoto kubwa. Hii inatokana na baadhi ya washirika kushindwa kukamilisha ahadi zao za imani kwa wakati, huku wengine wakihamia maeneo mengine bila kukamilisha ahadi hizo. Aliongeza kuwa mabadiliko ya mawasiliano kwa baadhi ya washirika yamefanya iwe vigumu kuwafikia.
Licha ya vikwazo hivyo, TAG MCC imedhamiria kusonga mbele. Mpango wa uinjilisti kwa mwaka 2026 unatarajiwa kupangwa katika kikao cha Desemba mwaka huu. Mchungaji Kiongozi ametoa wito kwa washirika kuendelea na moyo wa utoaji na kukamilisha ahadi zao ili kuwezesha injili kusonga mbele zaidi.

## SHUHUDA

# BAADHI YA MATENDO YA ROHO MTAKATIFU KWENYE HUDUMA YA INJILI YA 'MWENGE GOSPEL RUNNERS' 2025

### USHUHUDA WA MAMA HELENA ALIVYOSHINDA HUKUMU YA KIFO NA KUPATA UPONYAJI WA AJABU

Kanisa linamtukuza Mungu kwa ajili ya uponyaji wa kipekee wa Mama Helena (pichani) wa kijiji cha Mwakashanhara, Tabora. Kwa muda wa miezi sita, mama huyu alikuwa akisumbuliwa na tatizo la mkono ambalo lilikuwa na historia ya 'laana' katika familia yao; ambapo kila aliyepata changamoto hiyo na kutibiwa kwa sindano alifariki dunia.



Pichani Mama Helena akimshukuru Mungu kwa uponyaji.

Baada ya kufanyiwa maombi ya ukombozi, Mama Helena aliweza kupata matibabu hospitalini, ambapo alichomwa sindano, akivunja mwiko wa mauti uliokuwa ukiitesa familia yake. Hadi sasa, Mama Helena ni mzima wa afya na anaendelea kumtumikia Mungu kwa uaminifu.

## MBINU ZA ADUI KUZUIA ELIMU ZASHINDWA: USHUHUDA WA ELIZABETH MABULA



Pichani Elizabeth Mabula Mungu alimfungua kwa vifungo.

Binti Elizabeth Mabula (pichani), mkazi wa Puge mkoani Tabora, ameshuhudia ukuu wa Mungu baada ya kukombolewa kutoka katika vifungo vya giza vilivyokuwa vikizuia masomo yake. Tangu akiwa darasa la saba, Elizabeth alikumbwa na matatizo ya miguu yaliyopelekea mlipuko wa mapepo yaliyodai wazi kuwa dhumuni lao ni kumzuia asisome.

Hata hivyo, baada ya kufanyiwa maombi ya ukombozi, nguvu za giza zilimsitiri na kumuacha huru. Leo hii, Elizabeth si tu anaendelea na masomo, bali amefanikiwa kufaulu vizuri, akithibitisha kuwa hakuna mpango wa adui unaoweza kushinda kusudi la Mungu katika maisha ya mwanadamu.

## IBAGA YASHUHUDIA NGUVU ZA MUNGU: VILEMA NA VIFUNGO VYASAMBARATIKA

Nguvu za Mungu zilitembea kwa namna ya kipekee katika kijiji cha Ibaga, Singida. Kijana Gunda (picha haikuweza kupatikana mara moja), aliyekuwa akiteswa na ulevi uliokithiri pamoja na ugonjwa wa kifafa, alipokea uponyaji wa papo hapo baada ya kufanyiwa maombi. Uhai wake umerejea na sasa ni mshirika hai kanisani.

*Inaendelea ukurasa wa tano...*

*Inatoka ukurasa wa nne*

Aidha, ishara na maajabu vilitawala mkutano huo, ikiwemo ukombozi wa binti mmoja aliyekuwa akitoroka kwa nguvu za mapepo; alikamatwa baada ya kukimbia mita 200 na kufunguliwa kwa jina la Yesu. Hakika, mkono wa Bwana haujapunguka!


## FELISTA; NILIKUWA SIWEZI KUHISI KITU CHOCHOTE NIKIGUSA, LAKINI SASA NASIKIA NA KUONA PIA.

Ushuhuda wa Binti Felista (pichani) kutoka Ilongelo, Singida, unakumbusha nguvu ya huduma ya ukombozi. Akiwa amefungwa na pepo zilizosababisha usikivu duni na uono hafifu, Felista alipokea mguso wa Mungu uliovunja kila kifungo. Baada ya maombi ya ukombozi, alifunguliwa kikamilifu na kurejeshewa afya yake. Tunamtukuza Bwana kwa ajili ya nuru ya Kristo iliyomwangazia binti huyu na kumtoa gerezani.



Pichani Binti Felista wa Singida akimshukuru Mungu kwa uponyaji.

## MUNGU AFANYA OPERESHENI BILA KISU: USHUHUDA WA AJABU WA JANETH MAYALA



Pichani Janeth Mayala Mungu alimponya uvimbe tumboni.

Janeth Mayala (pichani), mkazi wa kijiji cha Gharambo, Lushoto mkoani Tanga, ameshuhudia nguvu ya uponyaji ya Mungu inayopita akili za kibinadamu. Baada ya kusumbuliwa na uvimbe tumboni kwa muda mrefu, Janeth alipewa rufaa ya kufanyiwa upasuaji mkubwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Hata hivyo, kabla ya kufika hospitalini, mkono wa Bwana ulimfanyia "upasuaji wa kimbingu" kupitia maombi ya ukombozi yaliyomuweka huru kutoka kwenye nguvu za giza. Wiki mbili baadaye, Janeth alielekea jijini Dar es Salaam kwa ajili ya vipimo vya kabla ya upasuaji, ambapo madaktari walistaajabu kukuta uvimbe huo umetoweka kabisa. Leo hii, Janeth ni mzima wa afya na ni ushuhuda hai wa ukuu wa Mungu!

## HUDUMA YA UPENDO: TIMU YA INJILI YAFIKISHA TABASAMU NA MATUMAINI KITUO CHA AFYA MKUZI

Katika kuonesha kuwa injili ya Kristo inahusu roho na mwili, timu ya injili ya Mwenge Gospel Runners (pichani ukurasa wa sita) ilipata wasaa wa kipekee wa kutembelea Kituo cha Afya cha kijiji cha Mkuzi, Muheza mkoani Tanga.

*Inaendelea ukurasa wa sita...*

*Inatoka ukurasa wa tano*

Mbali na kuwafariji wagonjwa kwa neno la Mungu, timu hiyo ilifanya maombi maalum ya uponyaji kwa wagonjwa waliolazwa na kutoa neno la faraja kwa madaktari na wauguzi. Huduma hii iligusa mioyo ya wengi na kuacha tabasamu la matumaini mapya kwa wagonjwa pamoja na watumishi wa kituo hicho, wakitambua kuwa Mungu yu pamoja nao katika kipindi cha udhaifu.



Timu ya Injili ya Mwenge Gospel Runners ilipotembelea Kituo cha afya cha Mkuzi, Muheza Tanga.

## USHINDI DHIDI YA VIFUNGO VYA GIZA: MAMA WA KILINDI AFUNGULIWA



Mama huyu Kutika Kwamba, Tanga Yesu alimkomboa na mateso.

Mama mmoja mkazi wa kijiji cha Kwamba, Kilindi mkoani Tanga (pichani) ameshuhudia ukuu wa Mungu baada ya kukombolewa kutoka kwenye kifungo cha mateso ya kiroho yaliyodumu kwa muda mrefu. Mama huyo, ambaye aliwahi kuolewa na mganga wa kienyeji kabla ya kutengana, alikuwa akisumbuliwa na matukio ya kutisha ya 'maluweluwe' na kuhisi kitanda chake kikipinduka nyakati za usiku.

Baada ya kufanyiwa maombi ya ukombozi na timu ya uinjilisti, nguvu za giza zilimwachia na kumuacha huru kabisa. Leo hii, mama huyo anaishi kwa amani, bila hofu wala mateso ya maluweluwe, akithibitisha kuwa nuru ya Kristo ni kubwa kuliko giza lolote.

## USHINDI WA AJABU TUNGULI: KIJANA ROBERT AFUNGULIWA KUTOKA KWENYE VIFUNGO VYA GIZA

Kijana Robert (A*liyekaa kwenye picha ukurasa wa saba*) mkazi wa kijiji cha Tunguli, Kilindi mkoani Tanga, amekuwa ushuhuda hai wa nguvu za Mungu baada ya kukombolewa kutoka kwenye changamoto ya akili na ugonjwa wa kifafa uliomtesa kwa muda mrefu.

*Inaendelea ukurasa wa saba...*

*Inatoka ukurasa wa sita*

Katika hali ya kutaabisha, Robert alikuwa akipatwa na mashambulizi yaliyompelekea kupoteza fahamu na kujiendesha kwa namna isiyo ya kawaida, ikiwemo kukimbilia mashambani. ya kufanyiwa maombi ya ukombozi na timu ya injili, nguvu za giza zilizokuwa zikimtesa zilisambaratika na kumuacha huru kabisa.

Leo hii, Robert amerejeshewa fahamu na afya yake, akimtukuza Mungu kwa ajili ya amani na uzima mpya aliopata.



Kijana Robert (Katikati) Kutoka Tunguli.

## MTEGO WA UDINI NA UFUATILIAJI: KWA NINI WAONGOFU WAPYA WANAREJEA WALIKOTOKA?

***Na Elizabeth Reuben, Mwenge***

RIPOTI ya ufuatiliaji wa mavuno ya injili kwa mwaka 2025 imebaini changamoto kubwa ya ustahimilivu wa waongofu wapya mikoani, baada ya takwimu kuonesha kuwa ni asilimia tisa (9%) pekee ya waliookolewa ndio wanaoendelea kushiriki ibada hadi sasa.

### Hali Halisi Katika Vituo

Uchunguzi uliofanywa na jarida hili katika vituo vyote nane umebaini hali ya sintofahamu. Kwa mujibu wa wachungaji wenyeji, akiwemo Mch. David (Mwakashanhara), Mch. Gerald (Puge), Mch. Mgelwa (Ibaga), na Mch. William Musa (Ilongelo), changamoto ya waongofu kurejea katika imani zao za awali imekuwa mwiba mchungu. Mchungaji Mollel wa kijiji cha Tunguli, ambaye ni miongoni mwa wachungaji waliofanya kazi na timu hiyo, alibainisha kuwa mazingira ya vijijini na shinikizo la kidini ni vikwazo vikuu.

Nimeendelea kutumia njia mbalimbali za ufuatiliaji, lakini tumekutana na roho ya udini iliyovishika vijiji hivi. Wengine wanarudi kwenye dini zao, na wengine wanatoa ahadi za kuja kanisani ambazo hawazitekelezi," alisema Mch. Mollel.

### Mchanganuo wa Takwimu kwa Kila Kijiji

| SN | KIJIJI | IDADI YA WALIOOKOKA | IDADI YA WANAOENDELEA |
|---|---|---|---|
| 1 | **Gharambo (Lushoto):** | 114 | 6 |
| 2 | **Tunguli (Tanga):** | 40 | 7 |
| 3 | **Mwakashanhara (Tabora)** | 38 | 4 |
| 4 | **Kwamba (Tanga):** | 38 | 2 |
| 5 | **Mkuzi (Tanga):** | 33 | 0 |
| 6 | **Ibaga (Singida):** | 26 | 7 |
| 7 | **Puge (Tabora):** | 21 | 2 |
| 8 | **Ilongelo (Singida):** | 16 | 2 |
| | **JUMLA** | **326** | **30** |

### Idara ya Uinjilisti Yatangaza Mikakati Migumu

Akizungumzia hali hiyo, Mkurugenzi wa Idara ya Uinjilisti, Ndugu Samuel Zayumba, amekiri kuwa changamoto hiyo imekuwa sugu na sasa inahitaji dawa ya kudumu. Zayumba ametoa onyo kuwa timu ya injili haitakuwa tayari kurejea kwenye maeneo ambayo mavuno yake hayalindwi.

"Mkakati wetu mpya ni huu; ikiwa wanaoendelea katika kituo fulani ni wachache au hakuna kabisa, timu haitarejea katika kijiji hicho. Hii ni hatua ya kuwahamasisha wachungaji wenyeji kuongeza jitihada za ufuatiliaji badala ya kutegemea mikutano pekee," alisisitiza Zayumba.

### Shukrani na Ombi la Kurejea

Licha ya takwimu hizo kulegalega, wachungaji wa vituo vilivyofikiwa wametoa shukrani za dhati kwa Mchungaji Kiongozi wa TAG Mwenge Christian Centre, Mch. Abdiel Mhini, uongozi wa kanisa, na timu ya Mwenge Gospel Runners. Wameomba kanisa lisiache kupeleka injili maeneo hayo ya vijijini kwani bado kuna kiu kubwa ya neno la Mungu, licha ya vita vya kiroho vilivyopo.
Mikutano hiyo nane iliyofanyika mwaka huu ni sehemu ya mpango mkakati wa kanisa kuhakikisha injili inafika maeneo yasiyofikika kwa urahisi, huku likiacha alama ya ukombozi kwa mamia ya watu.

## KONA YA WAIMBAJI

### MAPINDUZI YA UIMBAJI: IMANI CHOIR YAZINDUA ALBAMU YA 'LIVE RECORDING', YAANZA KUSAKA MILIONI 50 ZA USAFIRI

*Na Mwandishi wetu, Mwenge*



Kwaya ya Imani TAG Mwenge Christian Centre

KWAYA ya Imani ya Kanisa la TAG Mwenge Christian Centre (MCC), imehitimisha mwaka 2025 kwa kishindo baada ya kufanikiwa kutekeleza miradi miwili mikubwa ya huduma iliyogharimu zaidi ya shilingi milioni 26.
Mafanikio hayo yanahusisha ukamilishaji wa albamu mpya ya video yenye nyimbo tisa, pamoja na tamasha kubwa la uzinduzi lililolenga kuongeza nguvu katika ununuzi wa chombo cha usafiri (Coaster) kwa ajili ya huduma ya uimbaji.

Akizungumza na jarida hili kuelezea hatua hiyo muhimu, Mwenyekiti wa Imani Choir, Ndugu Danford Kitwana, amebainisha kuwa mwaka huu ulikuwa wa kipekee kwao kutokana na ukubwa wa malengo waliyojiwekea na jinsi yalivyotekelezwa kwa ufanisi



Kwaya ya Imani wakati wa uzinduzi wa santuri ya nyimbo zao

## Mapinduzi ya Uzalishaji: Mfumo wa 'Live Recording'

Ndugu Kitwana ameeleza kuwa mradi wa kurekodi video hiyo uliofanyika Aprili 11, 2025, ulikuwa na utofauti mkubwa wa kiufundi ikilinganishwa na kazi zilizopita. Safari hii, kwaya ilitumia mfumo wa kisasa wa uzalishaji unaojulikana kama 'Live Recording'.

"Tulijizatiti kuzalisha kazi bora itakayopenya kwenye soko la muziki nchini na kuwapa watazamaji kitu cha kipekee. Recording nzima ilifanyika hapa hapa kanisani kwa kutumia jukwaa la kisasa, skrini za LED (Background screens), na mifumo ya kisasa ya taa," alisema Kitwana.

Mradi huo wa kurekodi pekee uligharimu takribani shilingi milioni 20, ikihusisha uandaji wa audio, mavazi (sare), na malipo ya kampuni ya utayarishaji. Hata mwongozaji (Director) wa kazi hiyo, Ndugu Johnson Amigo, alikiri kuvutiwa na weledi wa kwaya hiyo akibainisha kuwa ni mara yake ya kwanza kufanya kazi yenye kiwango hicho cha juu na kwaya ya kanisa la TAG nchini.

## Uzinduzi na Ndoto ya 'Coaster'

Baada ya kazi hiyo kukamilika, mradi wa pili ulikuwa ni uzinduzi rasmi uliofanyika Oktoba 12, 2025. Shughuli hiyo iliyogharimu shilingi milioni saba, ilikuwa ni daraja la kuelekea lengo lingine kubwa: ununuzi wa gari aina ya Coaster kwa ajili ya huduma.
Katika uzinduzi huo, kwaya ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi milioni 20 (taslimu na ahadi), ikiwa ni sehemu ya lengo la shilingi milioni 50 zinazohitajika kwa ajili ya gari hilo. Kwa sasa, kwaya inaendelea na mikakati ya kuuza kazi hiyo kupitia mfumo wa flashi na mitandao ya kijamii ili kufikia lengo lililobaki.

## Shukrani na Malengo ya Huduma

Uongozi wa kwaya umetoa shukrani za dhati kwa Mchungaji Kiongozi wa TAG MCC, Mch. Abdiel Mhini na uongozi wote kwa kanisa pamoja na washirika wote kwa ushirikiano wa hali na mali.
Mwenyekiti Kitwana alisisitiza kuwa dhumuni la mradi huu si biashara tu, bali ni kupeleka neno la matumaini kwa ulimwengu, kuliimarisha kanisa, na kuitangaza vyema huduma ya TAG Mwenge Christian Centre.

## Historia ya Imani Choir

Imani Choir ina historia ndefu iliyoanza mwaka 1978, sanjari na kuanzishwa kwa kanisa la Mwenge MCC. Hadi sasa, kwaya imefanikiwa kutoa albamu tano za audio ambazo ni: Hata alipokuwa, Dunia hii siyo yangu, Kisha Nikaona, Mungu wetu halinganishwi na Moyo wa Ushuhuda (Albamu mpya).

Kwa upande wa video, kwaya sasa inajivunia jumla ya albamu tatu, ikiwemo hii mpya iliyozinduliwa mwaka huu ambayo inatazamwa kama kielelezo cha ukuaji wa kwaya hiyo kiroho na kitaaluma. Video zingine ni Kisha nikaona na Mungu wetu halinganishwi.

# KANISA NA WATOTO

## UWEKEZAJI KWA WATOTO: TAG MWENGE KUANZISHA SHULE YA AWALI NA KITUO CHA MALEZI IFIKAPO 2027

*Na Mwandishi Wetu, Mwenge*

KATIKA jitihada za kupanua wigo wa huduma kwa jamii, Kanisa la TAG Mwenge Christian Centre (MCC) limetangaza mpango mkakati wa kuanzisha shule ya kisasa ya kutoa huduma ya malezi na elimu ya awali (Daycare and Nursery School) ifikapo mwaka 2027.




(Walioketi kutoka kulia) Rev. Geofrey Paul wa kanisa la Zinga, Rev. Dr. Ezekiel Mbwilo ambaye ni Askofu wa jimbo la Ubungo, Rev. A. M Mhini - Mchungaji Kiongozi TAG Mwenge, Mke wa Mchungaji A.M Mhini na Mchungaji wa kanisa la watoto T.A.G Mwenge, Watoto na waalimu wa Kanisa la watoto T.A.G Mwenge.

Hatua hiyo inalenga kuimarisha misingi ya kiroho na kimwili kwa watoto, huku ikichangia katika utoaji wa elimu bora nchini.

Akizungumza na jarida hili kuelezea maono hayo, Mchungaji wa Kanisa la Watoto katika kituo hicho, Mch. Neema Mumghamba, alisema uamuzi wa kuanzisha shule hiyo umekuja baada ya idara yake kuona umuhimu wa kuwa na kituo kitakacholea watoto katika maadili imara tangu hatua za awali.

"Tumekuwa tukitoa huduma za kiroho kwa muda mrefu katika shule za msingi kama Shekilango na Mapambano, pamoja na shule ya sekondari ya Alpha. Sasa tumeona ni wakati muafaka kuanzisha shule yetu itakayotuwezesha kuzidi kuwafikia watoto wengi zaidi," alisema Mch. Neema.

### Huduma na Fursa za Ajira

Mch. Neema alibainisha kuwa uanzishwaji wa shule hiyo hautasitisha huduma ambazo kanisa limekuwa likizitoa katika shule nyingine za serikali na binafsi, bali utaongeza nguvu ya utendaji kutokana na uwepo wa walimu wengi wa watoto ndani ya kanisa hilo.

Mbali na kutoa elimu, mradi huo unatajwa kuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi kwa washirika. "Shule hii itatengeneza fursa za ajira rasmi kwa walimu wetu waliosomea taaluma hiyo (professionals). Watapata nafasi ya kutumia utaalamu wao, jambo litakaloboresha maisha yao," aliongeza.

## Uendelevu na Mkakati wa Eneo



Mchungaji wa Kanisa la watoto
Mch, Neema Mughamba

Akigusia uzoefu wa nyuma, Mch. Neema alisisitiza kuwa safari hii kanisa limejipanga kufanya mradi wa kudumu na wenye tija. Alibainisha kuwa Baraza la Wazee tayari limeunda kamati maalum inayofanya tathmini ya kina ili kuleta mapendekezo ya utekelezaji haraka iwezekanavyo.

Aliongeza kuwa eneo la Mwenge lilipo kanisa hili ni kitovu cha kimkakati (strategic centre) kinachofikika kirahisi, jambo linalotoa fursa kwa majirani na jamii inayozunguka kupata huduma hiyo kwa urahisi mara itakapokamilika kwa kuzingatia vigezo vyote vya Serikali kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii.

### Maono ya Kitaifa

Kwa upande wake, Mchungaji Kiongozi wa MCC, Mch. Abdiel Mhini, alisema mradi huu ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kanisa la TAG ujulikanao kama "Miaka 13 ya Moto wa Uamsho."

Mch. Mhini alifafanua kuwa mpango huo unahamasisha makanisa ya mahali pamoja kuanzisha shule za ngazi mbalimbali kuanzia chekechea hadi sekondari kama njia ya kuonesha upendo wa Kristo kwa jamii kupitia huduma ya elimu.

"Hii ni sehemu ya maono yetu ya kuhakikisha kanisa linakua kiroho na kutoa mchango unaoonekana katika nyanja za kijamii na kimaendeleo," alihitimisha Mch. Mhini.



Mch.Kiongozi Abdiel M. Mhini

## TAG MWENGE YAIMARISHA MALEZI YA KIROHO KWA WATOTO, YAVUKA MIPAKA HADI SHULENI

*Na Thiberia Sanga, Mwenge*

IDARA ya Watoto ya Kanisa letu la TAG Mwenge imefanya mageuzi makubwa ya kiroho kwa mwaka 2025 kupitia programu maalum za ufundishaji wa Neno la Mungu, kukuza vipawa, na kuimarisha maadili miongoni mwa watoto.

Chini ya usimamizi wa Mchungaji wa Watoto, Bibi Neema Mumghamba, idara hiyo imefanikiwa kutoa malezi ya kiroho kwa watoto kupitia makundi manne kulingana na umri: Chipukizi (miaka 13–17), Yusufu (miaka 9–12), Daudi (miaka 6–8), na Samweli (mwezi mmoja hadi miaka 5). Kwaya ya Sayuni imekuwa baraka kubwa, ikitoa huduma ndani ya kanisa na kualikwa maeneo mbalimbali. Hivi sasa tuko katika hatua za maandalizi ya kurekodi baadhi ya nyimbo zao ili kufikisha ujumbe mbali zaidi," alisema Mchungaji Mumghamba.

## Matunda ya Kiroho na Ukuaji wa Taaluma

Idara imeshuhudia ukuaji mkubwa wa kiroho ambapo watoto wengi wamejenga utamaduni wa kuwa na maombi wakati wa mahitaji yao, hususan katika vipindi vya mitihani. Hali hiyo imetajwa kuchangia ufaulu mzuri wa masomo yao shuleni.

Aidha, watoto wameonyesha uwezo mkubwa wa kukariri maandiko ya Biblia na kuwa chanzo cha kuwavuta wazazi wao kujiunga na ibada za kanisani.

Mchungaji Mumghamba aliongeza kuwa Kambi la Watoto lililofanyika Juni 2025 lilikuwa na mwamko wa kipekee. “Watoto walijifunza kwa kina na kufanyiwa majaribio ya kupima uelewa wao, na waliofanya vizuri walipewa zawadi. Tunatarajia kuwa na kambi lingine katikati ya mwezi Desemba mwaka huu.”

## Injili Mashuleni na Sikukuu ya Watoto

Katika hatua nyingine ya kipekee, idara imeweza kuvuka mipaka ya kanisa na kufikisha injili katika shule za msingi jirani za Mapambano, Shekilango na Shule ya Sekondari Alpha kupitia vipindi maalum vya dini.

Mafanikio hayo yalienda sambamba na Sikukuu ya Watoto ambapo watoto walishiriki kikamilifu kuongoza sifa, kuabudu, na kutoa neno la Mungu katika ibada zote, jambo lililoonyesha ujasiri na maandalizi mazuri kutoka kwa walimu 12 wanaojitolea katika idara hiyo.

## Changamoto ya Muda na Wito kwa Wazazi

Pamoja na mafanikio hayo, idara imebainisha changamoto ya watoto kuchelewa kufika kanisani siku za Jumapili, hali inayowafanya wakose vipindi muhimu vya mafundisho na badala yake kubaki nje wakicheza. “Yote yaliyotokea ni kwa utukufu wa Bwana, lakini tunawasihi wazazi kuwahimiza watoto kuheshimu muda wa ibada,” alisema Mwalimu Mkuu, Bi. Attu Alfred.

Mchungaji Mumghamba alihitimisha kwa kutoa wito kwa wazazi na walezi kutoishia kanisani tu, bali kuendeleza malezi ya kiroho nyumbani kwa kuwafundisha watoto neno la Mungu kwa bidii, akirejea agizo la maandiko katika Kumbukumbu la Torati 6:7.

# KONA YA VIJANA

## VIJANA MWENGE WANG’ARA, WATEKELEZA MALENGO YA MWAKA KWA KISHINDO

*Na Mwandishi wetu, Mwenge*

IDARA ya Vijana ya Kanisa la CAs Mwenge (Christ Ambassadors), imefanya mapinduzi makubwa ya kiutendaji baada ya kufanikiwa kutekeleza mipango yake 10 kati ya 13 iliyojiwekea kwa mwaka 2025, huku ikivuka lengo kwa zaidi ya asilimia 100 katika maeneo hayo. Mafanikio hayo yanatajwa kuwa ni kielelezo cha kukua kwa huduma na ushirikiano miongoni mwa vijana hao, ambao ndio injini kuu ya kanisa hilo wakijumuisha zaidi ya asilimia 75 ya washirika wote.

Akizungumza katika mahojiano maalum hivi karibuni, Mwenyekiti wa Idara hiyo, Bibi Happy Yese, amebainisha kuwa ni mipango mitatu pekee ambayo haikukamilika kikamilifu kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo mikutano ya injili, ibada ya shukrani, na uanzishaji wa miradi ya idara ambayo bado iko kwenye hatua ya tathmini.



Vijana wa CA's wa Mwenge Christian Centre walipokuwa wametembelea Bwawa la Minaki

"Katika mwaka wa 2025, tumefanikiwa kwa kishindo kufanya ushuhudiaji wa neno la Mungu, kushiriki matukio ya kijamii, kuandaa semina, maombi ya mfungo, na hata bonanza la michezo lililowakutanisha vijana wengi," alisema Bibi Yese na kuongeza:

"Pia tulifanikiwa katika mikesha ya maombi, kongamano la kusifu na kuabudu, na kufanya tathmini ya mara kwa mara. Katika malengo haya kumi, kila moja tumelifanikisha kwa zaidi ya asilimia 100."

## Changamoto zinazohitaji ufumbuzi

Licha ya mafanikio hayo ya kupigiwa mfano, Mwenyekiti huyo ameuomba uongozi wa kanisa kuangazia changamoto mbili kuu zinazokwamisha kasi ya ukuaji wa idara hiyo. Alitaja changamoto ya kwanza kuwa ni mwingiliano wa majukumu na fedha kwa vijana wanaoingia kwenye idara nyingine kama za kina mama (WWK) na wanaume (CMF).

"Kijana mmoja analazimika kutekeleza mipango ya WWK au CMF na wakati huo huo anatakiwa kutoa mchango kwa CAs. Hali hii inaleta mzigo mkubwa wa kifedha na mwingiliano wa utekelezaji," alibainisha. Aidha, alitaja suala la mahudhurio hafifu wakati wa siku za idara kuwa bado ni tatizo, ambapo takwimu zinaonyesha hayajafikia asilimia 50 licha ya jitihada za uboreshaji zilizofanyika.

## Wito wa mwaka 2026

Akirejea maandiko kutoka Isaya 60:1 na 1 Timotheo 4:12, Bibi Yese ametoa wito kwa vijana wote kuamka na kujiandaa kwa mwaka wa mageuzi zaidi.

"Mwaka 2026 ni mwaka wetu wa kuamka, kusimama imara katika imani na kuangaza katika huduma na maisha yetu ndani ya jamii. Tunataka kijana wa Mwenge awe kielelezo kwa wengine," alisisitiza.

Idara ya vijana inabaki kuwa uti wa mgongo wa kanisa hili kutokana na wingi wao, na uongozi unatarajia kuwa kuimarika kwa mipango yao kutaakisi moja kwa moja ukuaji wa kiroho na kimwili wa kanisa zima.

# KONA YA WANAWAKE

## WWK MWENGE YASHIRIKIANA NA FAMILIA KUBORESHA MADHABAHU YA KANISA

*Na Mwandishi Wetu, Mwenge*

IDARA ya Wanawake Watumishi wa Kristo (WWK) ya Kanisa la TAG Mwenge Christian Centre (MCC), imezindua awamu ya kwanza ya mpango kabambe wa kuboresha madhabahu ya kanisa hili ili kuifanya iwe na mwonekano wa kisasa na unaovutia. Katika mpango huo ulioanza Aprili mwaka huu, idara hiyo imeshirikiana na familia mbalimbali za washirika ambapo tayari maboresho makubwa yameanza kuonekana, ikiwemo uwekaji wa mbao za kuta (wall boards) na upanuzi wa eneo la madhabahu.

Mwenyekiti wa WWK Mwenge, Bibi Grace Bitegeko, ameliambia jarida hili kuwa lengo ni kuondoa 'wallpaper' za zamani na kuweka mapambo ya kisasa, kubadilisha kapeti, pamoja na kudhibiti mwangwi ili kuboresha sauti wakati wa ibada.

“Maboresho haya yanafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha. Hadi sasa, kupitia michango ya idara na familia za washirika, tumefanikiwa kuweka 'boards', kupanua madhabahu na kupaka rangi. Hatua inayofuata ni kubadilisha kapeti na kununua mapambo mapya,” alisema Bibi Bitegeko.



Chama cha wanawake (W.W.K) wa Mwenge Christian Centre, walipotembelea gereza la watoto lililopo Upamga Dar es salaam.

### Utume na Uangalizi wa Kiroho

Licha ya maboresho ya miundombinu, Bibi Bitegeko amebainisha kuwa idara hiyo imeendelea kutekeleza kusudi lake kuu la kuanzishwa kwa kumtegemeza Mchungaji Kiongozi kila mwezi.

Alieleza kuwa wanawake wamekuwa na utaratibu wa kutembelea nyumba ya mchungaji kwa ajili ya maombi na kutoa neno la faraja, jambo ambalo limeimarisha uhusiano wa kiutumishi kati ya idara na uongozi wa kanisa.

“Tunafuata mwongozo wa idara kwa kuhakikisha tunamshika mkono mchungaji wetu. Hii si tu kutoa sadaka, bali ni kuungana naye kiroho ili kumtia moyo katika majukumu yake mazito ya kulichunga kundi la Mungu,” alisisitiza.




Picha ikionyesha mradi wa sabuni ya maji ambayo ni Miradi ya kukuza uchumi kwa wanawake

### Mafunzo na Miradi ya Kiuchumi kwa wanawake.

Katika mwaka wa 2025, WWK iliwekeza nguvu kubwa katika mafunzo ya kiroho, ikiwemo mfululizo wa masomo kuhusu Roho Mtakatifu na umuhimu wa maombi ya uamsho. Mafunzo hayo yalitolewa na viongozi mbalimbali akiwemo Mzee wa Kanisa, Samwel Zayumba, na Mchungaji Neema Mumghamba.

Aidha, idara ilifanikiwa kuanzisha mradi wa kutengeneza sabuni ya maji, mradi ambao umeanza kusaidia wanawake kiuchumi huku soko lake kuu likiwa ni wanawake wa kanisa hilo.

### Huduma za Kijamii


Katika upande wa upendo na huruma, WWK iliendelea kuwa karibu na washirika kwa kutembelea wagonjwa mahospitalini na majumbani, pamoja na kufariji familia zilizofikwa na misiba au kupata baraka za watoto wachanga.

"Tumeunda kamati maalum ya kusimamia wageni na wongofu wapya ili kuhakikisha kila mshirika anayekuja kanisani anapata msingi mzuri wa kiroho," aliongeza Mwenyekiti huyo.
Bibi Bitegeko alihitimisha kwa kutoa wito kwa wanawake wote kutambua nafasi zao kama viungo katika mwili wa Kristo (1 Wakorintho 12:12-27), akiwataka kuheshimu neema za kila mmoja na kusimama katika zamu zao ili kulijenga kanisa moja la Mungu.

## KONA YA MAHUSIANO

### MAHUSIANO YA WANANDOA YANAYOMPENDEZA MUNGU

Ndoa ni taasisi takatifu iliyoanzishwa na Mungu mwenyewe tangu mwanzo wa uumbaji. Biblia inasema: "Kwa hiyo mwanaume atamwacha baba yake na mama yake, naye ataambatana na mkewe; nao watakuwa mwili mmoja" (Mwanzo 2:24). Hii inaonesha wazi kwamba mahusiano ya wanandoa si mpango wa kibinadamu tu, bali ni mpango wa Mungu unaokusudiwa kuakisi upendo, uaminifu na umoja.



Mahusiano ya wanandoa yanayompendeza Mungu yanajengwa juu ya misingi ya Neno la Mungu, upendo wa kweli, heshima ya pande zote, na uwajibikaji wa kiroho.

### 1. Upendo wa Kujitoa (Agape)

Upendo katika ndoa ya Kikristo haupaswi kuwa wa hisia tu, bali wa kujitoa na kujinyima. Mtume Paulo anawahimiza waume: "Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake" (Waefeso 5:25). Upendo huu ni wa kujali, kusamehe, na kutafuta mema ya mwenzi wako hata pale inapohitaji sadaka.

### 2. Heshima na Kuthaminiana

Mahusiano yanayompendeza Mungu hujengwa juu ya heshima ya pande zote. Biblia inasema: "Kila mtu na amthamini mwenzake kuwa bora kuliko nafsi yake" (Wafilipi 2:3). Mume na mke wanapaswa kuthaminiana kwa maneno, matendo na maamuzi, wakitambua kuwa kila mmoja ameumbwa kwa sura na mfano wa Mungu.



### 3. Mawasiliano ya Ukweli na Upendo

Mawasiliano mazuri ni msingi wa mahusiano imara. "Lakini kusema kweli katika upendo, tupate kukua hata tumfikie yeye katika yote" (Waefeso 4:15). Wanandoa wanapaswa kuzungumza kwa uwazi, kusikilizana kwa makini, na kutatua tofauti zao kwa hekima, bila lugha ya matusi, kejeli au hasira isiyodhibitiwa.

### 4. Uaminifu na Ahadi ya Ndoa

Uaminifu ni nguzo muhimu katika mahusiano ya wanandoa. Ndoa ni agano, si mkataba wa muda. "Aliyeyaunganisha Mungu, mwanadamu asitenganishe" (Mathayo 19:6). Uaminifu wa kimawazo, kihisia na kimwili humlinda mwenzi wako na huliheshimu agano la ndoa mbele za Mungu.

### 5. Maisha ya Kiroho ya Pamoja

Mahusiano yanayompendeza Mungu hayawezi kukua bila maisha ya kiroho ya pamoja. Kuomba pamoja, kusoma Neno la Mungu, na kuhudhuria ibada huimarisha umoja na kumweka Mungu katikati ya ndoa. "Kamba ya nyuzi tatu haikatiki upesi" (Mhubiri 4:12).

### 6. Kusameheana na Kuvumiliana

Hakuna ndoa isiyo na changamoto. Kusameheana ni hitaji la lazima. Yesu anasema: "Msameheane mara sabini mara saba" (Mathayo 18:22). Kusamehe huponya majeraha ya ndani na kulinda amani na mshikamano wa ndoa.

### 7. Uwajibikaji wa Kila Mwenza

Mungu amewapa wanandoa majukumu tofauti lakini yenye lengo moja: kujenga familia inayomcha Mungu. Waume wanaitwa kuongoza kwa upendo, na wake kuheshimu na kushirikiana (Waefeso 5:22–33). Uwajibikaji huu haupunguzi thamani ya yeyote, bali huleta uwiano na amani.

### Hitimisho

Mahusiano ya wanandoa yanayompendeza Mungu ni yale yanayomweka Kristo katikati, yanayojengwa juu ya upendo, heshima, uaminifu na maisha ya kiroho. Ndoa ya namna hii si tu baraka kwa wanandoa, bali pia ni ushuhuda hai kwa jamii na kizazi kijacho kuhusu upendo na mpango wa Mungu.

***Mungu na awape wanandoa wote neema ya kuishi mahusiano yanayompendeza, kwa utukufu wa jina lake. Amina.***



Washirika wa kanisa la Mwenge Christian Centre, wakiwa ibadani kanisani T.A.G Mwenge.

## RATIBA YA IBADA ZA KANISA

| JUMATANO | IJUMAA | JUMAPILI |
|---|---|---|
| **SAA 10.30 - 12.30 JIONI**<br>Ibada ya Mafundisho ya Neno la Mungu | **SAA 10.30 - 12.30 JIONI**<br>Ibada ya Maombi | **SAA 12.30 - 3.10 ASUBUHI**<br>Ibada ya Kwanza<br>**SAA 3.15 - 7.00 MCHANA**<br>Ibada ya Pili |

# TAHARIRI

## TUENEZE HABARI NJEMA NA KUHAKIKISHA MATUNDA YANAKAA

Kanisa la Yesu Kristo lilipewa agizo kuu lisilo na kikomo cha muda wala mahali: "Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi" (Mathayo 28:19–20). Hili ndilo agizo kuu la utume (Great Commission) na ndilo msingi wa kuwepo kwa Kanisa.

Katika dunia ya leo yenye changamoto za kiroho, kijamii na kiteknolojia, wito wa kueneza Injili ya Yesu Kristo haupaswi kupungua bali uongezeke kwa bidii, ubunifu na ujasiri. Kanisa halijaitwa kujifungia ndani ya kuta zake, bali "kukimbiza Injili"- kuifikisha habari njema kwa kila mtu, kwa kila njia halali, na kwa kila kizazi.

Hata hivyo, maandiko yanatukumbusha kwamba Injili haimalizikii kwenye kuhubiri tu, bali pia kwenye kukuza na kudumisha matunda. Yesu mwenyewe anasema: *"Nimewachagua ninyi mkapate kuzaa matunda, na matunda yenu yapate kukaa" (Yohana 15:16).* Hapa ndipo changamoto kubwa ya Kanisa la leo ilipo: ufuatiliaji wa waongofu wapya.
Suluhu ya Ufuatiliaji wa **Waongofu Wapya.**

## Suluhu ya Ufuatiliaji wa Waongofu wapya

Ili Injili izae matunda yanayokaa, Kanisa linapaswa kuimarisha mifumo madhubuti ya ufuatiliaji na malezi ya kiroho kwa waongofu wapya, ikiwemo:

**1.Programu Endelevu za Mafundisho (Discipleship):**
Waongofu wapya wafundishwe misingi ya imani, Neno la Mungu, maombi, na maisha ya Kikristo kwa mpangilio unaoeleweka na unaoendelea.

**2.Mfumo wa Malezi ya Kiroho (Mentorship):**
Kila muongofu mpya aunganishwe na mshirika aliyepevuka kiroho ili kumpa mwongozo, ushauri na mfano wa maisha ya Kikristo.

**3.Vikundi Vidogo vya Ushirika:**
Vikundi vya maombi, masomo ya Biblia, na ushirika wa karibu husaidia waongofu kujisikia kukubalika, kuthaminiwa, na kukua kiroho.

**4.Ushirikishwaji Katika Huduma:**
Waongofu wapya wahamasishwe kushiriki katika huduma mbalimbali za Kanisa kulingana na karama zao, ili wajione kuwa sehemu hai ya mwili wa Kristo.

**5.Ufuatiliaji wa Kiroho na Kijamii:**
Kanisa lisiwe tu mahali pa ibada, bali pia pa msaada wa kijamii, kiroho na kihisia, hasa katika nyakati za changamoto.

Kanisa linapokimbiza Injili kwa bidii na wakati huohuo likihakikisha matunda yanakaa, ndipo ufalme wa Mungu unapopanuka kwa uthabiti. Wito wetu si kuhesabu idadi ya waongofu pekee, bali kuona maisha yanabadilishwa na kudumu ndani ya Kristo.
Na kama asemavyo mtume Paulo: *"Mimi nilipanda, Apolo akanywesha; lakini Mungu ndiye aliyekuza" (1 Wakorintho 3:6)*. Basi na Kanisa liendelee kupanda na kunywesha kwa uaminifu, huku likimtegemea Mungu kuendeleza na kulikuza Kanisa lake, kwa utukufu wa jina lake. Amina.

## CHUMBA CHA HABARI:

**Mhariri wa Habari:** Danford Kitwana

**Msanifu wa Kurasa:** Reuben Msaki

**Wapiga Picha:** Augustino Mrema
Nicholous Matondane
Ibrahim Marwa

**Waandishi:** Elizabeth Reuben
Thiberia Sanga

**Mpiga Chapa:** ROM MEDIA TANZANIA

**MAWASILIANO:**
TAG Mwenge Chistian Centre (MCC)
P. O. Box 13049, Dar es Salaam.

Barua Pepe: mwengetag@gmail,com
Simu: 0755 341 644/0713 310 721

Mitandao ya Kijamii:
YouTube. : tag-mwengechristiancentre
Instagram : kanisani_tagmwenge_dsm
Facebook : kanisani Tag Mwenge